# HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha,

Telegram: Arusha.

Simu: 073 6500476,

Faksi: 250 3701.

Email:ded@arushadistrict.go.tz

Ukumbi wa Wilaya,

S. L. P. 2330,

**ARUSHA.**

**MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAMILIKA KATIKA HALMSHAURI YA ARUSHA MPAKA KUFIKIA 2016/2017-2017/2018.**

Baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyokamilika katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha katika sekata za Elimu, Afya na Maji.


## UPANUZI WA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA AFYA NDURUMA.

Ujenzi wa miundombinu hiyo umegharimu kiasi cha shilingi milioni 500, kiasi hicho cha fedha, kimetumika kujenga majengo mapya katika kituo hicho ikiwemo maabara, jengo la upasuaji, wodi ya mama na mtoto ' martenity ward' jengo la kujifadhia maiti, kichomea taka, vibaraza 'walk ways', nyumba ya mganga pamoja na umaliziaji wa jengo la ushauri nasaha 'CTC'.









**BARABARA YA MIZANZI -TIMBOLO**

Barabara ya Mianzini - Timbolo yenye urefu wa takribani Kilomita 9 imejengwa kwa kiwango cha lami urefu wa Mita 800 kwa gharama ya shilingi milioni 408 fedha za ambazo hutolewa na serikali kama ruzuku ya barabara.









**CHUO CHA UFUNDI MWANDETI.**

Chuo cha Ufundi Mwandeti kiko kata ya Mwandeti kinapokea wanafunzi waliomaliza elimu ya Msingi na kujifunza masomo ya Ufundi. Chuo hiki kinasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha chini ya Idara ya Elimu ya Msingi.








**HOSPITALI YA WILAYA OLTRUMET.**

Halmashauri ya Arusha ina jumla ya Hospitali 2 ikiwa moja ni ya binafis na moja ya serikali Hospitali ya Oltrumet.

Hospitali ya Oltrumet iko katika kata ya Oltrumet Mkabala na Radio Habari Maalumu umbali wa mita ….kutaka barabara ya Arusha –Namanga .

Huduma za wagonjwa wa nje, (OPD), Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto, Chanjo, Huduma za Uzazi wa Mpango, Huduma ya kujifungua na baada ya kujifungua, Huduma ya Kifua Kikuu, Huduma ya UKIMWI, Huduma za Afya kwa Wazee, Huduma ya Kulaza, Huduma za Elimu ya Afya, Huduma za Ushauri Nasaha, Huduma za Maabara na Huduma za Upasuaji.

Picha zifuatazo ni muonekano wa vituo 3 vya Afya vya serikali.















**VITUO VYA AFYA.**

Halmashauri ya Arusha ina jumla ya vituo 4 vya Afya ikiwa vituo 3 ni vya serikali na kituo kimoja cha binafsi.

Vituo hivyo vya Afya vinatoa huduma zifuatazo:-

Huduma za wagonjwa wa nje, (OPD), Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto, Chanjo,uzazi wa mpango huduma ya kujifungua na baada ya kujifungua, huduma ya Kifua Kikuu, Huduma ya UKIMWI, Huduma za Afya kwa Wazee, Huduma ya Kulaza, Huduma za elimu ya Afya, Huduma za ushauri nasaha, Huduma za Maabara na Huduma za Upasuaji.

Picha zifuatazo ni muonekano wa vituo 3 vya Afya vya serikali.

**KITUO CHA AFYA OLKOKOLA.**

Kituo cha Afya Olkokola kipo katika kata ya Lemanyata kinahudumia wananchi wa kata nzima ya Lemanyata yenye jumla ya watu 5,847 kutoka katika vijiji 2 na vitongoji 5 pamoja na wagonjwa kutoka kata za jirani.





**KITUO CHA AFYA NDURUMA.**

Kituo cha Afya Nduruma kipo katika kata ya Nduruma kinahudumia wananchi wa kata nzima ya Nduruma yenye jumla ya watu **12,042** kutoka katika vijiji **3** na vitongoji **11** pamoja na wagonjwa kutoka kata za jirani.









**KITUO CHA AFYA OLDONYOSAMBU**

Kituo cha Afya Oldonyosambu kipo katika kata ya Oldonyosambu kinahudumia wananchi wa kata nzima ya Oldonyosambu yenye jumla ya watu **2,770** kutoka katika vijiji 3 na vitongoji 8.









**HUDUMA YA ZAHANATI.**

Halmashauri ya Arusha ina jumla ya Zahanati 28 katika viji 28 vya Halamshauri ya Arusha, Ingawa Mpango wa serikali ni kuwa na zahanati katika kila kijiji, Halmashauri inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa zahanati ukilinganisha na idadi ya vijiji. Katika Mpango Mkakati (***Strategic Plan)*** wa miaka mitano kuanzi 2017/18 mpaka mwaka 2020/2021, Halmashauri inategemea kuwa na zahahnati katika kila kijiji kwa vijiji vyote 67.

Huduma ya afya katika Zahanati inapatikana mchana kwa muda wa kazi na huduma za dharura kwa maeneo ambayo kuna nyumba za watumishi wa afya wanaoishi eneo la karibu la zahanati.

Huduma za wagonjwa wa nje, (OPD), Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto, Chanjo,uzazi wa mpango huduma ya kujifungua na baada ya kujifungua, huduma ya Kifua Kikuu, Huduma ya UKIMWI, Huduma za Afya kwa Wazee, Huduma za elimu ya Afya, Huduma za ushauri nasaha pamoja na Huduma za Maabara. Picha zifuatazo ni muonekano wa zahanati za Halmashauri ya Arusha.

**ZAHANATI YA NDURUMA.**

Zahanati ya Nduruma ipo katika kijiji cha Nduruma kata ya Nduruma, Zahanati inahudumia wananchi wa kijiji kijiji cha Nduruma na vitongoji 4.





**ZAHANATI YA KISERIANI.**

Zahanati ya Kiseriani iko katika kijiji cha Kiserianio kata ya Mlangarini inahudumia wananchi kutoka katika kijiji cha kiseriani na votongoji vyake  tisa pamoja na wananchi kutoka kata za jirani za jiji la Arusha.










## ZAHANATI YA LIKAMBA

Zahanati ya Likamba iko katika kijiji cha Kiserianio kata ya Mlangarini inahudumia wananchi kutoka katika kijiji cha kiseriani na votongoji vyake  tisa pamoja na wananchi kutoka kata za jirani za jiji la Arusha.









## AHANATI YA LOSIKITO

Zahanati ya Losikito iko katika kijiji cha Losikito kata ya Mwandeti inahudumia wananchi kutoka katika kijiji cha Losikito na votongoji vyake.









**MRADI WA UJENZI WA MADARASA NA VYOO SHULE YA SEKONDARI OLJORO.**

Katika kutatua changamoto ya kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi kurundikana katika darasa moja, Serikali imejenga vyumba vinne vya madarasa kwa gharama ya **Tsh. 92,000,000.00** vyenye uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi mia mbili **(200)** kwa wastani wa wanafunzi **50** kwa darasa moja. Madarasa haya yalifunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani **Mhe. Kassim Majaliwa Kassim tarehe 08.12.2016.**








**CHOO CHA WANAFUNZI SHULE YA SEKONDARI YA OLJORO**

Serikali inahakikisha wanafunzi mwanasoma katika mazingira salama ya kiafya, Serikali kupitia miradi ya **CDG** imejenga choo cha matundu kumi kwa thamani ya **Tsh. 20,000,000.00 kwa ajili ya matumizi ya wananfunzi wa shule ya Sekondari Oljoro.**








**NYUMBA YA WALIMU SHULE YA SEKONDARI OLJORO.**

Katika kuhakikisha walimu wanapata mahali salama pa kuishi na karibu na eneo la shule serikali imejenga nyumba ya walimu yenye uwezo wa kuishi familia sita za walimu katika shule ya Sekondari Oljoro kata ya Laroi, mradi huo umegharimu kiasi cha **Tsh.102,225,939.00** fedha za **SEDP II.** Nyumba hii ilifunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa tarehe 08.12.2016.**













Mradi wa Ujenzi wa nyumba ya waalimu yenye sehemu mbili (2 in 1) shule ya Msingi Laroi kata ya Laroi wenye thamani ya **Tsh. 84,789,886.00** ikiwa **Tsh. 71,760,886.00** fedha za TASAF, **Tsh. 7,522,000.00** mchango wa Jamii na **Tsh. 5,507,000.00** mchango wa Halmashauri. Nyumba hii ni moja ya miradi ya iliyoibuliwa na wananchi na inatekelezwa na Mradi wa **TASAF awamu ya tatu.**









**BWALO LA CHAKULA SHULE YA SEKONDARI MLANGARINI.**

Shule ya Sekondari Mlangarini ni shuel ya Bweni ina wanafunzi wa kidato cha I – VI, katika kuhakikisha wanafunzi hao wanakuwa na sheemu nzuri ya kulia chakula Halmashauri kwa kushirikia na Wadau mbali mbali wa Maendeleo wa kata ya Mlangarini Serikalai imejenga Bwalo la chakula kama linavyooneka katika picha hapo chini.










**MABARA YA SAYANSI SHULE YA SEKONDARI MLANGARINI**
















**MRADI WA MAJI NDURUMA.**

Mradi wa Maji Nduruma ni miongoni mwa miradi ya Vijiji kumi iliyoanza utekelezaji wake mwaka 2006 kwa kufadhili wa Banki ya Dunia. Mradi huu umegharimu kiasi cha **Tsh. 854,030,182.20.** Mradi umekamilika na utahudumia jumla ya watu **12,042** wa vijiji vya Mzimuni, Nduruma, Marurani na Majimoto. Mradi huu umezinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Kassim kwenye kituo cha kuchotea maji cha Oldenderet tarehe 08.12.2016.





**MRADI WA MAJI OLMULO:**

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha inaendelea kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia wafadhili mbalimbali moja wa mradi huo ni **Mradi wa maji Olmulo katia Kata ya Oljoro.** Mradi wa OLMULO uliotekelezwa na shirika la **SIMAVI** kutoka Uholanzi kupitia shirika tekelezi la **CBHCC** kwa gharama ya **Tsh. 1,710,612,240/=.** Mradi wa maji **Olomulo** ulizinduliwa na **Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliji Mhandisi Isack Kimwele** tarehe 15.02.2017.









